

# YAI LANGU LA **PASAKA**

## MY EASTER EGG



**Umeona yai langu la pasaka?**

**Mimi natafuta yai langu la waridi.**

**Natafuta kila mahali.**

**Oh! Nimelipata!**

**Yai langu la Pasaka liko katikati ya majani.**



**Have you seen my Easter ergg?**

**I am looking for my pink egg.**

**I am looking everywhere.**

**Oh! I have found it!**

**My Easter egg is in the middle of the grass.**

**Nimepoteza yai langu la Pasaka.**

**Yai langu la njano.**

**Naomba unisaidie kulitafuta.**

**Oh! Nimeliona!**

**Yai langu la Pasaka lipo chini ya mti.**



**I have lost my Easter egg.**

**My yellow egg.**

**Please help me find it.**

**Oh! I have seen it!**

**My Easter egg is under the tree.**

**Yai langu la Pasaka linaweza kuwa wapi?**

**Yai langu jeupe.**

**Rafiki yangu, naomba nitafutie.**

**Oh! Lile pale!**

**Yai lako la Pasaka liko nje ya boksi.**



**Where could my Easter egg be?**

**My white egg.**

**My friend, please help me find it.**

**Oh! It's over there!**

**Your Easter egg is outside of the box.**

Nani ameona yai langu la Pasaka?  
Yai langu la rangi ya machungwa.  
Dada! dada! Njoo tulitafute wote.  
Oh! Hili hapa!  
Yai lako la Pasaka liko ndani ya kikapu.



Who has seen my Easter egg?  
My orange colored egg.  
Sister! sister! Come let's look for it together.  
Oh! It's right here.  
Your Easter egg is in the basket.

**Nimeweka wapi yai langu la Pasaka?  
Yai langu la madoadoa.  
Kaka, je ni wewe umelificha?  
Hapana! Labda tulitafute.  
Oh nimeliona!  
Yai lako la pasaka lipo pemberi ya kitanda.**



**Where have I put my Easter egg?  
My polkadot egg.  
Brother, did you hide it?  
No! Maybe let's look for it.  
Oh I have seen it!  
Your Easter egg is beside the bed.**

**Unajua yai langu la Pasaka lilipo?  
Yai langu la kijani. Bibi, nitafutie tafadhalli.  
Sawa. Nitaangalia kila mahali.  
Oh! Nimelipata. Hili hapa!  
Yai lako la Pasaka lipo karibu na maua.**



**Do you know where my Easter egg is?  
My green egg. Grandma, please help me search for it.  
Ok. I will look everywhere.  
Oh! I have found it.  
Your Easter egg is close to the flowers.**

**Nani anaweza kutafuta yai langu la Pasaka?  
Yai langu la rangi nyeusi.  
Mimi nimechoka kulitafuta.  
Oh! usikate tamaa rafiki yangu.  
Yai lako lipo nyuma ya sungura.**



**Who can find my Easter egg?  
My black egg.  
I am tired of looking for it.  
Oh! Don't give up my friend.  
Your egg is behind the bunny.**

**Yai langu la Pasaka liko wapi?  
Yai langu la rangi ya dhahabu.  
Je lipo mbele, nyuma, ndani au nje ya nyumba?  
Oh! Nimelipata!  
Hili hapa mbele ya nyumba.**



**Where is my Easter egg?  
My golden egg.  
Is it in front, behind, inside or outside the house?  
Oh! I have found it!  
It's here! Right in front of the house.**

Nani ameficha yai langu la Pasaka?

Yai langu la kijivu.

Oh mdogo wangu! Umeangalia uvunguni mwa kitanda?

Jaribu kuinama. Lile pale!

Yai lako liko chini ya kitanda.



Who has hidden my Easter egg?

My grey egg.

Oh my little sister! Have you looked under the bed?

Try bending. It's over there!

Your egg is under the bed.

**Mayai yangu ya Pasaka yana nini ndani?**

**Ngoja niyapasue ...**

**Yai moja lina gari na lingine lina mdoli.**

**Mengine yote siri yangu. Sitaki kukuambia!**

**Jaribu kuotea tuone kama utapata!**



**Do you know what's inside my Easter egg?**

**Let me crack them ...**

**One egg has a car and another one has a dolly.**

**All the rest is my secret. I don't want to tell you!**

**Try to guess and see if you get it right!**

# ZOEZI

Chagua jibu sahihi – Pick the right answer

1. Yai maana yake kwa kingereza ni nini?

- a. Basket
- b. Bunny
- c. Egg


2. Ndani ya yai Kuna nini?

- a. Kuku na bata
- b. Mtoto na mti
- c. Gari na mdoli

3. Siri maana yake ni nini kwa kiingereza ?

- a. Run
- b. Bend
- c. Secret

# Watoto Mini Book Series by.....



# swahiliKIDS

To get more free & fun Swahili Learning resources visit



<https://www.swahilikids.com>



@kiswahiliKIDS



@swahiliKIDS



@swahili.KIDS